# KUFANYWA MWANA

**Kuwekwa katika nafasi ya Mwana (Waefeso 1:3-6)**

Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa Baraka zote za Rohoni katika Ulimwengu wa Roho ndani yake Kristo kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya Ulimwengu ili tuwe Watakatifu watu wasio na hatia mbele zake katika pendo, kwa kuwa alitangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawa sawa na Uradhi wa mapenzi yake. Na asifiwe Utukufu wa neema yake ambayo ametuneemesha katika hiyo mpendwa.

## Kumbuka kwamba kufanywa wana kuna hatua tatu:-

Kwa sababu sisi ni wana uzao wa Kifalme wa Ibrahimu Mungu ametuma Roho ya Mwanae katika mioyo yetu ambaye analia aba yaani baba kwa hiyo sisi siyo watumwa tena **(Watumishi)** wa dhambi na kutoamini lakini tu wana ***(Warumi 6:- 16-23 ; Yohana 16:9)*** na kama tu wana tu warithi pia wa Mungu, warithio pamoja na Kristo **(Wagalatia 4:6-9 ; 3:-7 ; Warumi 8:-6-17)** kwa sababu hiyo tumeweza kushuhudia uzazi wetu mpya kwa sababu sisi tulikuwa wana **(Mbegu)** za Mungu kwa maana ni mbegu za Mungu ambazo zinaweza zikazaliwa tena (1) ***(Mathayo 13:38)*** siyo kwa kule kuzaliwa kwamba ndio tunafanywa mbegu lakini sisi tulikuwa mawazo yake ya milele (sifa za Mungu, mbegu za Mungu, ***(Luka 8:- 11)*** ambao sasa tunadhihirishwa katika mwili hikiitwa wana wa Mungu ***(Yohana 3:-1-8)*** kwa kule kuzaliwa upya tulipokea Roho ya kufanywa wana kwa neema (2) ***(Warumi 8:14-17)*** na mtu yoyote aliyezaliwa kutokana na mbegu ile isiyoharibika ya neon la Mungu ni sehemu ya Mungu ***(1 Petro 1:23 ; Yakobo 1:18,*** hapo sasa tunafanywa wana tunapokelewa kama wana katika familia ya Mungu kupitia Yesu Kristo ***(1 Petro 1:18 – 19 ; Ufunuo 1: 5 - 6)*** ambae alikuwa ni Mungu mwenyewe na akafanyika mwili ili aweze kufa kwaajili ya familia yake iwezayo kuokolewa na sasa tumetiwa mhuri ndani yake baada ya kuamini neon la kweli ***(Yohana 16 : 13 ; Wakolosai 1 : 5)*** pamoja na Roho Mtakatifu wa ahadi ambae ni arabuni ya urithi wetu mpaka wakati wa ukamilifu wa kulipwa ile gharama ya ukamilifu yote sifa ya Utukufu wake ***(Waefeso 1:13 – 14).***

Lakini kule kufanywa mwana kwako sio kuzaliwa kwako ; kufanywa mwana kwako ni kuwekwa mahali pako (3) kwa maana unazaliwa kwa Roho wa Mungu katika Utukufu wa Mungu lakini umechaguliwa kimbele kufanywa mwana kuwa kwa mahali pako tunakuwa watoto kwa kuzaliwa, na kule kuzaliwa mara ya pili na kule kubadilishwa kwenye Roho Mtakatifu wewe hujaokolewa mpaka umempokea Roho Mtakatifu ***(Luka 22 : 31 – 32 ) (2)*** ili mradi motto Yule bado ni motto hakuna tofauti kati yake na mtumwa ingawaje ni Bwana wa vitu vyote
***(Wagalatia 4 : 1 ; 1 Wakorintho 3 : 1 – 8 )*** sasa mwana akizaliwa yeye ni mwana mara tu anapozaliwa inakuwa ni mwana katika ile nyumba lakini bado hakuwa na urithi wowote mpaka

amefika mahali ambapo amejithibitisha mwenyewe kuwa ni mwana na sasa akithibitisha kuwa ni mwana, sasa hapo alifanywa mwana katika familia ana nafasi sawa na baba yake (4).

Tunaona kwamba tabia yake ndio inamfanya yeye afanywe mwana mwenye mamlaka kama alionyesha tabia nzuri au hapana, sasa Mungu amekuchukua wewe katika mwili wa Kristo
***(1 Wakorintho 12 : 13 )*** sasa anafanya mazuri baada ya kujithibitishia mwenyewe kujitakasa mwenyewe kwa mwenendo wako mzuri, mtiifu kwa Roho Mtakatifu, haijalishi dunia inasemaje hapo sasa Mungu anamuita mwana wa pembeni ya udhihirisho haitaji kusema jambo lolote juu ya hilo naona jambo Fulani limetendeka akimueka mwanae mahali pake, akimuweka katika utaratibu wa vitu vile vile yeye anakuwa na Mamlaka neno lake linakuwa ni kama malaika mkuu zaidi Yule mwana amefanywa kwa mwenye mamlaka akawekwa mahali pa juu akawekwa hapa mavazi yake yakabadilishwa rangi zake zikabadilishwa baba yake akawa na sherehe akisema huyu ni Mwanangu kuanzia hapa na kuendelea yeye ni mtawala, yeye yuko juu ya urithi wangu wote vyote nilivyo navyo ni vyake hiyo ni sawa hapo sasa tunaweza tukarudi nyuma tena kwenye jambo lile lile elah, elah, elohm, elohim unaona yeye ni aishie peke yake halafu unakuja hapa kupitia Jehova ambae amefanya kitu Fulani akampa mwanadamu mamlaka juu ya dunia. Tunangojea nini sasa? Udhihirisho dunia inaugua ***(Warumi 8:19-22) (2)***

Mungu amelificha kutoka kwenye macho ya wenye hekima na akili na akaahidi kulifunua kwa wana wa Mungu wa awakati wa mwisho ***(Mathayo 11:25)*** wakati wana wa Mungu watakapoweza kudhihirishwa, wakati wana wa Mungu walipoweza kufurahi nae kabla ya kuwekwa misingi ya dunia ***(Ayubu 38 :7 )*** wakati wa ufunuo mkuu wa Uungu siku za mwisho atadhihirisha mambo haya kwa wana wa Mungu, unajua maandiko yanafundisha hilo na tuko hapo hiyo ndiyo sababu Mungu anafungua mambo haya kwetu Mungu anawaleta watoto wake katika udhihirisho anaonena kupitia viwango vya mwisho vya mwanadamu yoyote akiingia katika viwango vya ufunuo na akivileta huku chini (5)

Je hiyo ni sawa? Kusubiri Mungu akijaribu kuweka Kanisa lake katika nafasi ya yeye kujidhihirisha mwenyewe akitafuta mmoja ambaye anaweza akatenda nae kupitia kama hivi kusema pale pana Roho wangu akitiririka kwa uhuru. Lile pale ile ile kumweka hapa naweza kumuweka hapa naweza kumuweka hapa nimfanye mwana mwenye mamlaka. Kumuweka, kumdhihirisha, kumchukua yeye hapa nje na kufanya sherehe juu yake nimtembelee yeye na malaika nimwambie jambo Fulani ***(Waebrania 1:14)*** kama amesema ukweli sasa kama ana jaribu kufanya tu kitu Fulani haitatenda kazi hapana!! Hapana!! Hiyo haitatenda kazi tumekuwa na mengi ya namna hiyo lakini namaanisha kudhihirishwa kwa wana wa Mungu mahali ambapo Mungu anajidhihirisha yeye mwenyewe na kumtuma yeye nje yeye anaendelea mbele anachosema ni kweli, anachofanya anamdhihirisha Kristo utawezaje kuona hilo kwa namna anavyokaa na neno yuko sawa na neno unaona? Hivyo ndivyo unavyoweza kuwajua watu wote ni kwa namna wanavyosimama kwa neno kama hawasemi sawa sawa na neno hakuna uzima ndani yao ndivyo biblia inavyosema unaona? Waache hawa (2).

Mara nyingine tena mtu anapolithibitisha hili na Mungu anampenda anamchukua nje mahali Fulani akiwa pekee yake pamoja na malaika anafanya jambo kwaajili yake ana muinua pale uweponi pa Mungu na anampa vipawa namjaza anamuweka pale nje huo ndio wakati tunaoishi ndani yake. (6)

Sasa ulijaribu kumuona Musa? Yule mtenda miujiza mkuu ambae aliwatoa wana wa Israel akiwapitisha katika jangwa akiwapeleka nchi ya ahadi lakini uliona kwamba hakuwapa urinzi yeye hakuweza kuwapa urithi wao; aliwapeleka mpaka karibu na ile nchi nani Joshua aliyewagawanyia watu ile nchi hiyo ni sawa? Na Yesu Kristo alilileta Kanisa mpaka mahali ambapo milki yao ilikuwa dhahiri kwao na walipewa hiyo ilikuwa wavuke tu Yordani lakini Roho Mtakatifu ndiye anae liweka Kanisa katika utaratibu , Yoshua wa leo analiweka Kanisa katika utaratibu akimpa kila mmoja wao karama akimuweka mahali, sehemu, na sauti yake inakuwa ni Mungu anazungumza kwa Yule mtu wa ndani ambae Kristo alimuokoa Roho Mtakatifu sasa unapata hilo kulielewa tunaingia hapa kwenye kitabu cha Waefeso ni kwa njia hiyo, hiyo analiweka Kanisa mahali ambapo linapaswa kuwa sasa Joshua aliwaweka wao kwenye nchi ya kimwili ya asili, sasa Roho Mtakatifu analiweka Kanisa mahali pale katika mahali ambapo ni urithi wao (3).

Ule waraka kwa Waefeso unalinganishwa kikamilifu kabisa na kitabu cha Joshua katika agano la kale (7) Roho Mtakatifu ambae ni neno la Mungu aliyepakwa mafuta, linatutaka sisi tuishi kiungu kila siku katika wiki nzima, tukitenganishwa sisi na mambo ya ulimwengu
***(Yohana 6:63; 2 Wakoritho 6:14 – 18)*** yeye ni Joshua wetu wa kimbinguni, kiongozi wetu wa kiungu wa siku hii nay eye pekee ndiye awezae kutuchukua katika urithi wetu hata katika nafasi zetu ndani ya Kristo hapo tu tunapowekwa mahali petu katika Kristo – Neno lililopakwa mafuta tunaingia katika pumziko lake ***(Waebrania 4:5 -6) (8).***

Hiyo ndiyo tatizo la watu leo hawawezi kysubiri Roho Mtakatifu halisi, kuliweka Kanisa mahali pake inabidi waumbe kitu Fulani wafanye jambo Fulani wawe na uthibitisho wa kunena kwa lugha, kupata watu zaidi katika Kanisa mambo haya yote ya upuuzi badala ya kumngojea Bwana kwa udhihirisho halisi za ufufuko wa Yesu Kristo ajitambulishe mwenyewe na mkumbuke kwamba Roho Mtakatifu si kwenda mpaka aliponiambia nifanye hilo nilikuwa nangojea hili asema Bwana, mpaka nilipopata hii asema Bwana hiyo ndiyo tofauti, unaona? Sasa hiyo inafanya tofauti ndio Paulo alisubiri neno la Mungu alikuwa nasongwa katika Roho kufanya tu kile anachotaka Mungu. Yeye alikuwa mfungwa wa Yesu Kristo marafiki kama tunaweza tu tukawa wafungwa!! (10)

**Kwanini tumepewa Roho Mtakatifu?** Yeye ni hazina ya Mungu ya upendo katika mioyo ya wanaume na wanawake kutii ***(Matendo 5 : 32) (11)*** Tuna kiongozi mmoja tu ambae ni Roho

Mtakatifu kwa sababu ni yeye tu atakae kuchukua katika nchi yetu nchi ya Roho Mtakatifu ujumbe wa sasa hii neno la Mungu (13) ***(Zaburi 16 : 6 ; 2 Wakoritho 5 : 4).***

Hatutakuwa na pumnziko mpaka tumemiliki urithi wetu, lazima uwe kile ulicho na siku zote ubakie kile ulicho, sasa tunajua tunaishi sasa katika wakati wa kufanywa wana wenye mamlaka wakati wa Efeso na Roho Mtakatifu anatuweka sisi katika neno katika nafasi katika Roho Mtakatifu nchi ya nyumbani ambayo pia anaitwa kanaani ya Kiroho sasa tunaona ile hali ya kuwekwa mahali petu katika urithi wetu sio kule kuzaliwa mara ya pili kitu cha kibinafsi cha kufanywa wana wenye mamlaka katika nafasi zetu ndani ya Kristo kinafanyika ili kufanya kazi ya baba kutimiza neno lililoahidiwa la Mungu ***(Ufunuo 22 :17 ;10 :8 -11 ; Mathayo 17 :1 -8 ). (13)***

Na kila mtu anapochukua nafasi yake kile Mungu alichomuita kufanya na akisimama mpaka mwisho wa njia (14)

Mungu anapozungumza na mtu ana imani na nashauku na anakua na kusudi Mungu anapozungumza na mtu anampa kusudi anampa shauku, Mungu anapozungumza na mtu anampa imani ya kufanya hilo kukamilisha au kufikia lile lengo katika maisha yake ambalo Mungu amemuitia kufanya, ametuita sisi kuwa katika Kanisa la Mungu, Amina (13).

Wakati huo unapokuja wakati Kanisa limepata upendano wa ndugu, Kanisa linapopata uzuri wa utakatifu ninapopata mahali pake katika Kristo nitawaita washiriki wengine wa mwili njooni mfurahi pamoja nasi Mungu anapenda Kanisa limpende yeye (15).

Ili kuwezesha huku kufanywa wana wa Mungu alifanya jambo Fulani la ajabu kupitia mihuri saba ***(Ufunuo 6: 10:1 -7)*** siri za Biblia zilifanywa zijulikane kwa sababu hiyo sisi kama wana wake pia tukiitwa bibi arusi tutashuhudia ule udhihirisho uliosubiriwa na kuingia ya wana, nafasi ndani ya Kristo tumefika mahali sahihi tumezaliwa mahali petu na kujazwa na Roho Mtakatifu ni neno la Mungu. (16)

Tufungue (***Warumi 8: 22 – 23)*** nafikiri ni nzuri sana kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia naugua pamoja navyo vina utungu pamoja hata sasa. Wala si hivyo tu ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani ukombozi wa mwili wetu unaliona hilo? Viumbe vyote vinaugua alisema Paulo kila kitu kinaugua na hata sisi wenyewe alisema Paulo, tunaugua pia kwa maana tunasubiri ukombozi wa miili yetu ***(Warumi 8: 19 -22)*** lakini sasa imekuwa hivyo kwa miaka hii yote mpaka sasa tunao arabuni urithi wetu ***(Waefeso 1 : 13- 14)*** Oh jamani tuna nini tulichonacho, tuna ushahidi kwamba Mungu anaishi, tuna ushahidi kwamba Mungu yupo pamoja nasi, tuna ushahidi kwamba Mungu hakutuacha sis, sisi ni wake na yeye ni wetu kwa sababu katika miili yetu hii sasa imekuwa ni maskani ya Roho Mtakatifu wa Mungu ambae analia aba, baba na hakuna kitu

kinachoweza kukuondoa hilo, asili haina hilo, lakini bado tunaugua pamoja nayo kwa sababu hatujapokea ukamilifu wa ukombozi wetu lakini tunayo arabuni kwamba tumenunuliwa juu kutoka kwenye mambo ya ulimwengu na sasa tunakuwa wana na binti wa Mungu tunapaswa kuwa watu wa nama gani ooh jamani tunapofikiri hili, fikiri hilo, sasa tunae arabuni, Roho zetu zinaugua kwaajili ya ukamilifu wa kufanywa wana wenye mamlaka ***(Warumi 8:23)*** lakini sasa tunayo arabuni ya hilo kwa kadri ya tulivyopokea Roho Mtakatifu ambao ni arabuni ya ukamilifu wa kufanywa wana wenye mamlaka au ukamilifu wa ukombozi wetu jinsi lilivyozuri nalipenda sana hilo, tunasubiri ukamilifu wa kufanywa wana lini? Wakati wa ufufuo wa kwanza hapo ndipo miili yetu itakapobadilishwa kutoka kwa hivi viumbe viovu na tutakuwa na mwili kama mwili wa kwake wa utukufu kwa maana tutamuona kama alivyonasi tutakuwa kama yeye ***(Wafilipi 3:20-21)*** atakapooneka ***(1 Yohana 3:2 )*** tutakuwa na mwili kama wa kwake, mwili wa utukufu uliotukuzwa na majaribu yote na mahangaiko yote ya maisha yatapotea na kuwa kama kaungu kadogo na kutupwa mbali lisionekane tena na haya maskani ya dunia ambayo katika haya tunaugua, tukisubiri hiyo arabuni ya ukombozi mkamilifu katika ukamilifu wake uje lakini sasa katika maskani yake hi madogo kitu kina kuna kitu kinatuambia kwamba tumeinuliwa juu kwa umbali Fulani ***(Waefeso 2:6 )*** amina. Arabuni ni nini? ***(2 Wakoritho 1:21-22)*** ni yale malipo ya chini ambayo yanashikilia kitu, ndiyo arabuni (7).

Wakati Kanisa linaugua chini ya kukandamizwa na dunia ya nje kwa kumuamini Yesu Kristo kwamba ilr ahadi ya Roho Mtakatifu iko tu kama vile ni kitu halisi kwetu kama ilivyokuwa Pentekonte walivyougua na kulia katika uchungu wa kuzaa, lakini wanapozaliwa na kuwekwa mahali katika Ufalme wa Mungu hapo sasa Roho Mtakatifu ameweka wengine katika Kanisa kwa mitume, manabii, wengine walimu, wengine wachungaji, wengine wainjilisti
***(Waefeso 4:11)*** halafu ametoa katika hao kunena kwa lugha kutafsiri lugha, maarifa, hekima karama za uponyaji aina zote za miujiza ***(1 Wakoritho 12:7 – 11, 28 – 30) (7)***

Roho Mtakatifu Yule Yule aliyewaokoa Walutheri alie watakasa mettodishi aliyewabatiza Wapentekonte sasa hivi analiweka Kanisa katika utaratibu wa kuja kwa Bwana Yesu itakapokuwa na nguvu sana kiasi kwa ule mwili utakuja katika kundi hili la Kanisa ambao litakuja kuwavuta waliobaki kaburini tutakuwepo ufufuko ***( Wakorintho 15 : 50 – 57)*** hiyo ndiyo sababu ya Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu ni nini? Bila ya sisi wao wasingeweza kukamilishwa ***(Waebrania 11:39 – 40)*** waliishi siku moja chini ya hilo tunaishi katika siku nyingine wakati adui akija kama mafuriko Roho wa Mungu atainua kiwango cha kumpinga ***(Isaya 59:19)***

Mungu ananisubiri mimi na wewe kanisa lina nisubiri mimi na wewe wakati wa wa kufanywa wana wakati mungu akatufanyia sisi ukamilifu wake,nguvu zake ufufuki wake kwamba kanisa na kristo vinakuwa pamoja anaonekana miongoni mwetu akifufua watu na kwenda kwenye unyakuo sasa tutaenda kusema,tutaonyesha ninyi baada ya muda mfupi wale walio jazwa na roho Mtakatifu wanaenda kwenye unyakuo wale walio bakia miongoni mwa wafu hawakuishi tena

kwa muda wa miaka elfu ***(Ufunuo 20-5)*** hiyo ni kweli ni watu tu waliojazwa na roho mtakatifu ndio pekee walio enda kwenye unyakuo. (6)

Mungu alipasa afunue ili mihuri saba iliyo katika madhehebu nilikuwa siku zote kinyume nayo, lakini kwenye madhehebu unaweza bibi harusi siyo bibi harusi wa kidhehebu hawezi akafanya hivyo ni kinyume na neno lake alifungua zile siri saba pale akazionyesha akija leta yale mambo yaliyo kuwa yamefichwa tangu kuweka misingi ya urimwengu –ziweze kufunuriwa katika siku za mwisho-kwa wana wa mungu wanaileta hiyo mbele ya macho ya watu ili waone iko pale ninyi sasa ambao siyo bibi harusi wa kidhehebu..18…

Anga lenye mawingu na dhoruba za maisha siyo ishara za kukataliwa na mungu kadhalitea anga angavu na maji yaliyo tulia siyo ishara za upendo na kukubali kukataliwa kwa kila mmoja wetu ni kupatia tu kwa huyu mpendwa ,upendo wake ni wa kuchagua ambao arikuwa nao kwaajili yetu kabla ya kutowekwa misingi ya ulimwengu anatupenda sisi ndio lakini tutajuaje tutajua kwa sababu kasema hivyo na akadhahilisha hilo,kwa sababu ametununua sisi tuwe wake na akatupa sisi roho mtakatifu wake akituweka sisi kama wana nitathibitishaje upendo wangu kwake kwa kuamini kwa kuamini alichosema na kuendelea mbele kwa furaha katikati ya majaribu ambayo katika hekima yake anayaruhusu yatokee…1…

**NUKUU ZA KINGEREZA**

1. *Wakati wa Kanisa la Symirna (Nyakati saba za Kanisa) UK.152,118*

*(2) Kufanywa wana sehemu ya tatu (60-0522M) aya 151,66,74,85-86,72,159*
*(3) Kufanywa wana sehemu pili (60-0518) aya 114,19*
*(4) Msikie yeye (60-0806)aya E38A*
*(5) Uzao wa nyoka (58-0928E) aya 149*
*(6) Roho Mtakatifu ametolewa kwa kusudi gani (59-1217) aya 54,49,00*
*(7) Kufanywa wana sehemu ya kwanza (60-0515E) aya 28,50*
*(8) Ufunuo sura ya tano sehemu ya pili (61-0618) aya 61*
*(9) Lile neno lililonenwa ndio mbegu ya asili (62-0318) aya 59*
*(10) Paulo mfungwa wa Yesu Kristo (63-0717) aya 110-111*
*(11) Kujaribu kumtendea Mungu kazi (65-1127B) aya 232*
*(12) Maagizo ya Gabriel kwa Daniel (61-0730 M) aya 133*
*(13) Inachukua nini kushinda kutokuamini kote (60-0729) aya E-73*
*(14) Kufanywa wana sehemu ya nne (60-0522E) aya 49*
*(15) Kule kuja kwa pili kwa bwana (57-0417) aya 71*
*(16) Wakati wa mavuno (64-1212) aya 188*
*(17) Ufunuo sehemu ya kwanza nyoka aliyejeruhiwa (61-0611) aya 103-108*
*(18) Muungano usioonekana wa bibi arusi wa Kristo (65-1125) aya 303*

---

Jiwe la kiroho la kujengea No. 1 mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald
Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax (+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098.*